# 11,280 wafundishwa ufugaji wa samaki

Na John Nditi, Morogoro

KITUO cha ukuzaji viumbe maji cha Kingolwira kilichopo Morogoro kimetoa mafunzo kwa wananchi 11,280 kutoka mikoa mbalimbali kuhusu ufugaji samaki kwa njia ya kisasa.

Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Ukuzaji Viumbe Maji kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk Imani Kapinga, alisema hayo kituoni hapo wakati akieleza utekelezaji majukumu ya kituo tangu kilipoanzishwa.

Dk Kapinga alisema katika kipindi cha mwaka 2010 hadi 2020 ambacho wananchi hao walipata mafunzo,kituo hicho pia kilizalisha vifaranga (mbegu) vya sato 6,026,832 vilivyosambazwa katika mikoa ya Morogoro, Iringa, Pwani, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mbeya, Ruvuma, Rukwa, Dodoma , Singida , Tabora, Unguja, Mwanza na Arusha.

"Sehemu ya vifaranga (mbegu za samaki) vilivyozalishwa vilitumika kupandikiza kwenye malambo na mabwawa ya asili katika mikoa ya Morogoro, Pwani, Singida na Iringa," alisema.

Kapinga alisema wanavyuo 1,450 kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Chuo cha Uvuvi Mbegani na Chuo cha Uvuvi Kunduchi kwa nyakati tofauti walipatiwa elimu kwa vitendo katika kituo hicho.

Alisema kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti ya Uvuvi (TAFIRI), SUA na UDSM, kituo hicho kimefanya tafiti zinazohusu ufugaji samaki.

Dk Kapinga alisema katika kutatua changamoto zinazokikabili kituo hicho, katika mwaka wa fedha 2020/2021, serikali ilitenga Sh milioni 262.3 kwa ajili ya kufanya ukarabati wa jengo la ofisi, kitoleshi na kibanda cha walinzi.

Alisema ukarabati huo unatarajiwa kuboresha mazingira ya kazi, kuiongezea uzalishaji wa vifaranga (mbegu za samaki), na kuimarisha ulinzi wa kituo hicho.

# TARILI yaomba kusaidiwa kuwasomesha watoto wa Dk Chaula

UONGOZI na Bodi ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TARILI), imeanzisha michango itakayo wasaidia watoto wa aliyekuwa Kaimu mkurugenzi wa Taasisi hiyo kanda ya kati Dk Haruna Chawala na Neema Mwasanganga waliofariki Machi 5, mwaka huu baada ya gari lao kusombwa na maji katika korongo la Shaban Robert.

Tukio hilo lililotokea katika wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma limezua taharuki na majonzi kwa wananchi na viongozi mbalimbali ikiwemo wa Taasisi hiyo.

Familia hiyo imeacha watoto wadogo wawili, Angela Chawala mwenye umri wa miaka minane ambaye ni mwanafunzi wa darasa nne na Adison Chawala mwenye umri wa miaka sita ambaye ni mwanafunzi wa darasa la kwanza.

Kwa mujibu Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa TARILI, Dk Jonas Kizima wameamua kuwasaidia watoto hao kutokana na mazingira ya wazazi wao walivyokufa na kuwataka Watanzania wote kuwasaidia watoto hao ili waweze kufikia ndoto zao kimasomo na kimaisha.

Aidha Dk Kazima alisema tayari wamesha wafungulia akaunti watoto hao, na taasisi pamoja na watumishi wameshachanga kiasi cha Sh 1,748,500 na kimewekwa kwenye akaunti za watoto hao na michango inaendelea.

Kwa upande wa mwenyekiti wa bodi ya TARILI, Profesa Sebastian Chenyambuga alisema pamoja na kuendelea kuomboleza na kusikitika jambo la muhimu ni kuwasaidia watoto walioachwa na marehemu ili kufikia malengo yao.

" Ni kweli mtumishi wetu amefariki sawa, lakini kuendelea kusikitika tu haitasaidia, tunataka kuwaona watoto hao wanasonga mbele bila kupoteza ndoto zao sisi tumeanzisha tuu tunawaomba Watanzania wote watuunge mkono kuwasaidia watoto hao." alisema Profesa Chenyambuga

Profesa Chenyambuga alisema akaunti za watoto hao wamezifungua katika benk ya NMB ambapo mtoto wa kwanza ni Angela Chawala akaunti namba 5161670011158213 na mtoto wa pili ni Edson Chawala 51616700160771.

Mkurugenzi wa shule ya St Austin iliyopo wilayani hapa ambako ndiko watoto hao walikokuwa wakisoma Siana Lema amejitolea kusomesha watoto hao na kuwapatia kwa mahitaji ya shule hadi hapo watakapomaliza elimu yao ya Msingi.

Pia familia iliyowasimamia kwenye ndoa ya Chawala na mkewe na kuwasimamia kwenye ubatizo wa mtoto Angela ambayo ni familia Jonathan Sarakikya amejitolea kuwatunza watoto hao na hadi sasa wanaishi kwao .

Scanned with CamScanner

# Wafugaji waomba kuwekewa utaratibu mzuri

**Na Mwandishi Wetu, Rufiji**

WAFUGAJI wilayani Rufiji Mkoa wa Pwani, wameiomba serikali kuweka utaratibu mzuri utakaowafanya wafugaji kuwa na maeneo ya ufugaji, ili kuondokana na changamoto zinazowakabili hivi sasa zikiwemo kutakiwa kuondoka kwenye maeneo wanayofugia sasa.

Wamesema wamekuwa wakiisikia serikali inavyoelezea kutengwa maeneo kwa ajili ya wakulima na wafugaji, hivyo wameomba maeneo yao yaainishwe na kuwekwa miundombinu rafiki kwa mifugo, badala ya kuambiwa wahame bila mpangilio maalumu.

Wakizungumza na waandishi wa habari wilayani hapa, wafugaji hao walisema maisha yao kwa sasa yamekuwa na changamoto nyingi, ikiwemo kusumbuliwa huku wakiambiwa waondoke wilayani Rufiji.

Akizungumza kwa niaba ya wafugaji na viongozi wezake Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Wilaya ya Rufiji na Kibiti, Deus Ndaki alisema changamoto kubwa inayowakabili wafugaji wilayani hapa ni ya kutakiwa kuondoka bila kujua wanakwenda wapi.

Alisema siku za nyuma, kulikuwa na maeneo yaliyotengwa na yalikuwa yanachukua ng'ombe 6,000 lakini hivi sasa kuna ng'ombe 70,000.

Mwenyekiti huyo alisema, mahali wanakoambiwa waende hakuna miundombinu kama majosho lakini pia kuna miti mikubwa na ng'ombe hawali miti hiyo.

"Tunatoa ombi na kuishauri serikali iweke utaratibu mzuri utakaowezesha wafugaji kutosumbuliwa na kukamatwa kila kukicha," alisema.

Wakati huo huo, alisema pamoja na changamoto hizo wafugaji wa maeneo hayo wameanzisha ushirika wao na wamepata usajili ili kuanza kufuga kisasa na hatua hiyo, watabadilika kwani wao si mawe ni binadamu.

Scanned with CamScanner

# Waziri Mashimba abaini ubadhirifu mnada wa mifugo Upili- Igunga

NA MWANDISHI WETU

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amemsimamisha kazi ofisa anayesimamia Mnada wa Mifugo wa Upili, ulioko Wilayani Igunga, Mkoani Tabora, Juma Athuman, kwa tuhuma za ubadhirifu wa fedha za mapato.

Hatua hiyo aliichukua juzi, alipotembelea mnada huo ili kuangalia ufanisi wake, ambapo alibaini kutokuwepo nyaraka za kumbukumbu ya mifugo inayoingia na kutoka katika mnada huo kwa kipindi cha miaka minne mfululizo.

Alisema kukosekana kwa kumbukumbu hizo, kumetoa mwanya wa upotevu wa mapato, hivyo kuisababishia serikali hasara ya mamilioni ya fedha na kusisitiza kwamba, jambo hilo halikubaliki.

"Naagiza uongozi wa halmashauri, kumwondoa kazini mara moja Ofisa Afya ya Mifugo, Mohamed Kifamba, askari polisi wote waliokuwa wakisimamia mnada huo, nao waondolewe mara moja, OCD shughulikia hilo," alisema.

Licha ya kusimamishwa kazi watuhumiwa hao, Waziri Mashimba, aliagiza vyombo vya dola kufanya uchunguzi wa kina juu ya tuhuma hizo za ubadhirifu wa mapato ya serikali kwa kipindi chote cha miaka minne ili sheria ichukue mkondo wake.


"Kila siku ya mnada, fedha nyingi zinakusanywa, lakini hazionekani, zinaingia mifukoni mwa watu, hili halikubaliki na serikali haiwezi kufumbia macho vitendo vya namna hiyo, kwa kuwa vinaikosesha mapato mengi sana," alisema Waziri.

Alimwagiza Katibu Mkuu wa wizara hiyo, kupeleka wataalamu wilayani humo ili kuchunguza mapato ya mnada huo, yaliyopotea katika kipindi chote hicho ili hatua za kinidhamu ziweze kuchukuliwa, ikiwemo wahusika kulipa fedha hizo.

Wakati utaratibu wa kumpata ofisa mwingine atakayesimamia mnada huo ukiendelea, Waziri Mashimba, alimteua Haidari Mwinyihaji, kusimamia mnada huo kwa muda.

Alimtaka Mkurungezi wa halmashauri hiyo, kupeleka haraka mtaalamu mwingine atakayesimamia mifugo katika mnada huo, huku akimtaka OCD wa wilaya hiyo naye kupeleka askari wengine.

UKAGUZI



**WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (kulia), akikagua vitabu vya kumbukumbu ya idadi ya mifugo inayoingia na kutoka katika mnada unaosimamiwa na wizara hiyo, Upili, Wilaya ya Igunga, mkoani Tabora, juzi.**

Scanned with CamScanner

# Afa akidaiwa kuchomwa mkuki na wafugaji Handeni

Rajabu Athumani, Mwananchi
rathmani@mwananchi.co.tz

**Handeni.** Mtu mmoja amefariki dunia na wengine wawili kujeruhiwa baada ya kuchomwa kwa mikuki na watu wanaodhaniwa ni wafugaji waliovamia kijijini kukomboa mifugo yao iliyokuwa imekamatwa baada ya kula mazao shambani.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Blasius Chatanda amesema tukio hilo lilitokea Jumapili Aprili 5, baada ya walinzi watatu wa mgambo katika Kijiji cha Kwasunga kukamata ng'ombe waliokuwa wamevamia shamba na kula mazao ya mkulima kwenye eneo hilo.

Alisema majira ya usiku siku hiyo, kundi la wafugaji lilivamia kijiji hicho na kuanza kuwashambulia walinzi hao, ambapo waliwachoma mikuki sehemu mbalimbali za miili yao na kisha kuchukua mifugo yao na kutokomea.

**AGIZO LA MKUU WA WILAYA**

Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Toba Nguvila ameagiza kuanza msako wa wakulima na wafugaji walioingia Handeni bila utaratibu ili kudhibiti wafugaji na mifugo yote iliyoingia kinyume na utaratibu wilayani humo.

Chatanda alisema siku ya Jumatano Aprili 7, mlinzi mmoja wa mgambo, Yusuph Boli alifariki dunia akiwa anaendelea na matibabu katika Kituo cha Afya Mkata, ambapo wanakijiji wengine wawili walilazwa kwa matibabu.

"Boli alijeruhiwa kichwani na leo (jana) alfajiri amefariki dunia wakati akiendelea kupatiwa matibabu," alisema.

Chatanda alieleza kuwa Jeshi la Polisi limeanza msako wa kuwatafuta waliohusika na tukio hilo, kwani wamefanya makosa kwa kujichukulia sheria mkononi.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kwasunga, Omari Yusuph alisema tatizo lililopo kwenye maeneo mengi wilayani Handeni ni kwamba hakuna udhibiti wa mifugo kwenye mipaka, hali inayofanya mifugo kutoka maeneo ya jirani kuingia wilayani humo mara kwa mara.

Kadhalika, Adam Philipo, mkazi wa Kwasunga alishauri viongozi ngazi ya vijiji wapokonywe mamlaka ya kupokea wageni na mihuri, kwani wao ndio wanahusika zaidi kupokea wageni na likitokea tatizo hukanusha kuhusika.

Scanned with CamScanner